TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY



# JARIDA LA HABARI

TOLEO NAMBA: 007 DISEMBA, 2020

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

## SERIKALI YAKABIDHIWA RADA YA TATU ILIYOPO MTWARA UK. 2



## DC HANDENI: TAARIFA ZA HALI YA HEWA NI NYENZO MUHIMU KWA UCHUMI WA TAIFA LETU UK. 3

## TMA YATOA MWELEKEO WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2020 - APRILI 2021) UK. 4



# SERIKALI YAKABIDHIWA RADA YA TATU YA HALI YA HEWA ILIYOPO MTWARA

Dar es Salaam,

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekabidhiwa rasmi rada ya tatu ya hali ya hewa ambayo imefungwa katika Kilima cha Mbae, Mtwara. Makabidhiano hayo yamefanyika baini ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na mzabuni Entrerprise Electronics Corporation (ECC) kutoka Marekani kwa usimamizi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) kwenye Makao Makuu ya TMA, Tarehe: 18 Disemba 2020.

“Serikali imekamilisha upatikanaji wa Rada ya tatu ya hali ya hewa ikiwa ni mwendelezo wa usimikaji wa rada saba nchini, Rada hii ni ya kisasa inauwezo wa kuangazia kwa zaidi ya kilomita 500, hivyo tunauhakika wa kupata taarifa za hali ya hewa za usahihi na kwa wakati” alisema hayo Mhandisi Aron Kisaka, Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) wakati wa makabidhiano rasmi.




*Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhandisi. Aron Kisaka (wa kwanza kushoto), akishuhudia makabidhiano ya rada ya tatu ya hali ya hewa iliyopo Mtwara yaliyosainiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi (wa katikati) na mwakilishi kutoka kampuni ya Enterprise Electronics Corporation (EEC), Mhandisi. James Youngblood, Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*



*Picha ya rada mpya ya hali ya hewa iliyopo mkoani Mtwara.*

“Leo tumepokea taarifa ya hitimisho ya namna mradi ulivyokamilika, uzinduzi rasmi wa rada hii utafanyika na viongozi wa ngazi ya juu mara watakapo kuwa tayari kufanya hivyo, hivi sasa utaendelea kutumika kwaajili ya majaribio”. Aliongezea Mhandisi Kisaka.

Aidha aliongeza kwa kuishukuru Entrerprise Electronics Corporation (ECC) kwa ushirikiano waliouonesha na kuwasihi kuendelea kutoa ushirikiano ili kukamilisha mradi wa rada nyingine inayotarijiwa kufungwa Jijini Mbeya.

Naye mwakilishi wa Entrerprise Electronics Corporation (ECC) kutoka Marekani Bw. Edwin Kasanga alihakikishia Serikali kuwa wataendelea kutoa ushirikiano wa dhati ili kuhakikisha miradi inayoendelea inakamilika kwa wakati kulingana na makubaliano ya mikataba.

JARIDA LA HABARI

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# DC HANDENI: TAARIFA ZA HALI YA HEWA NI NYENZO MUHIMU KATIKA UCHUMI WA TAIFA

**Tanga,**

Wananchi wa Handeni, mkoani Tanga wametakiwa kutumia taarifa za hali ya hewa katika kuleta mafanikio ya kiuchumi kwa Taifa letu. Hayo yalizungumzwa na Mgeni Rasmi ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Toba Nguvila wakati akifungua rasmi Warsha ya Kuongeza Uelewa wa Upatikanaji, matumizi na Usambazaji wa Taarifa za Hali ya Hewa iliyofanyika katika ukumbi wa FDC, Handeni, Tarehe: 19 Disemba 2020.



*Mgeni rasmi ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Toba Nguvila akizungumza kwa kusisitza wakati akifungua warsha ya kuongeza uelewa wa upatikanaji, kutafsiri matumizi na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa katika ukumbi wa FDC, Handeni*

“Kutafsiri taarifa za hali ya hewa kunahitaji utaalamu, wananchi wengi hawana utaalamu huo, hivyo kupata nafasi ya warsha hii ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa yanafanyika na kuleta mafanikio ya kiuchumi kwa Taifa letu, Dkt. Kabelwa yeye mwenyewe amekuwa akituma taarifa kupitia mitandao ya kijamii ili zitufikie wanahandeni kwa wakati, na taarifa ya msimu wa Vuli mwaka huu imeeleza uwepo wa mvua chache, naendelea kusisitiza tutumie vizuri nafasi hii”. Alizungumza Mhe. Nguvila.

Mhe. Nguvila aliendelea kuzungumza kuwa elimu ya kuongeza uelewa imekuja wakati muafaka kwa kutambua kuwa takribani asilimia 90 ya wananchi wa Handeni ni wakulima, hivyo kupata taarifa sahihi na kwa wakati hususan msimu wa kilimo ni jambo la muhimu sana.

“Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli ameiboresha sana Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kwa kuwapatia mitambo ya kisasa ili kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinazotolewa kwa umma ni za uhakika na usahihi wa hali ya juu”. Alisisitiza Mhe. Nguvila

Awali, wakati akizungumza kwenye ufunguzi, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu TMA ambaye pia ni Mkurugenzi wa Huduma za Utabiri, Dkt. Hamza Kabelwa alimshukuru Mgeni Rasmi kwa kufungua warsha hiyo ambayo ni mara ya piliu, ambapo ya kwanza ilifanyika mwaka 2017 na kuwataka washiriki wote kuendeleza ushirikiano wa kuhakikisha matumizi ya taarifa za hali ya hewa yanaleta tija.

“Warsha hii imejumisha wadau mbalimbali wakiwemo madiwani, watendaji kata, maafisa ugani, walimu, wakulima na RedCross, nawaomba wadau wote kuendelea kuwa mabalozi wa TMA”. Alifafanua Dkt. Kabelwa

Naye, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji-Handeni, Bw. Kenneth Haule alifurahishwa na uwepo wa warsha hiyo na kueleza kuwa hali ya hewa ni muhimu sana, hasa ikizingatiwa kilimo ni uti wa mgongo.

Kwa upande wa Katibu Tawala, Handeni, Bw. Mashaka Mgeta alisema, hivi sasa kumekuwa na changamoto ya mabadiliko ya hali ya hewa, hivyo ni vyema kutekeleza maelekezo ya wataalamu wa hali ya hewa ili kuweza kukabiliana na changamoto hizo.

Akifunga warsha hiyo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji-Handeni aliwataka madiwani wote kuifanya elimu ya hali ya hewa kuwa ajenda kuu katika utekelezaji wa majukumu yao, na kuishukuru TMA kwa jitahada zake.

Warsha hiyo imeandaliwa na TMA kwa kushirikiana na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) na Shirika la Kimataifa la Korea (KOICA).

4

# JARIDA LA HABARI

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# TAARIFA MAALUM

## UTABIRI WA MVUA ZA MSIMU (NOVEMBA, 2020 – APRILI, 2021)




*Mwelekeo wa mvua za Msimu (Novemba, 2020 hadi Aprili, 2021)*

### 1.1 Mwenendo wa Mvua za Vuli (Oktoba-Disemba), 2020

Msimu wa Vuli kwa miezi ya Oktoba hadi Disemba 2020 katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua (Mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Mara, Manyara, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro, Pwani (ikijumuisha kisiwa cha Mafia) pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) unatarajiwa kuendelea kama ilivyotabiriwa hapo awali ambapo maeneo mengi yalitarajiwa kupata mvua za chini ya wastani hadi wastani. Aidha, mvua za nje ya msimu zinatarajiwa katika mwezi Januari 2021.

### 1.2 Mwelekeo wa Mvua za Msimu Novemba, 2020 hadi Aprili, 2021 (NDJFMA 2020-2021)

Kutokana na mifumo ya hali ya hewa inayotarajiwa (kama ilivyoelezwa katika kipengele cha 2 cha taarifa hii), mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nyanda za juu kusini magharibi, kanda ya kati pamoja na Pwani ya kusini.
Aidha, maeneo ya magharibi yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Hata hivyo, mvua nyingi zinatarajiwa kunyesha katika nusu ya pili ya msimu.

Mvua za Msimu ni mahususi katika maeneo ya magharibi mwa nchi, kanda ya kati, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi, ukanda wa pwani ya kusini pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro. Maeneo haya yanapata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, unaoanza mwezi Novemba hadi Aprili ya mwaka unaofuata. Maelezo ya kina juu ya mwelekeo wa mvua hizo za msimu ni kama ifuatavyo:

**i. Kanda ya Magharibi: (Mikoa ya Kigoma, Tabora na Katavi):**

Mvua za wastani hadi chini ya wastani zinatarajiwa kunyesha katika mkoa wa Kigoma pamoja na magharibi mwa mikoa ya Tabora na Katavi. Mashariki mwa mikoa ya Tabora na Katavi mvua zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani. Mvua hizi zinatarajiwa kuanza kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi Novemba, 2020 katika mikoa ya Tabora na Katavi na kusambaa kusini mwa mkoa wa Kigoma katika wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Novemba, 2020. Mvua hizo zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**ii. Kanda ya Kati: (Mikoa ya Singida na Dodoma):**

Mvua katika maeneo haya zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani na zinatarajiwa kuanza katika wiki ya kwanza hadi wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2020. Mvua zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**iii. Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Iringa, Njombe, pamoja na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Mvua za wastani hadi juu ya wastani zinatarajiwa katika maeneo mengi ya nyanda za juu kusini magharibi isipokuwa mkoa wa Rukwa unatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2020 na zinatarajiwa kuisha wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021.

**iv. Pwani ya kusini na maeneo ya kusini mwa nchi: (Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma):**

Mvua zinatarajiwa kuanza wiki ya pili ya mwezi Novemba, 2020 na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika maeneo mengi. Mvua zinatarajiwa kuisha kati ya wiki ya pili na ya tatu ya mwezi Aprili, 2021 katika mkoa wa Ruvuma na wiki ya nne ya mwezi Aprili, 2021 katika mikoa ya Lindi na Mtwara.




**Ramani 1: Kushoto: Mwelekeo wa mvua za *Msimu* (Novemba, 2020 –Aprili, 2021) na Kulia: Wastani wa muda mrefu wa mvua za *Msimu* (1981 -2010).**

***Izingatiwe kuwa matukio ya vipindi vifupi vya mvua kubwa yanaweza kujitokeza hata katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za chini ya wastani.***

## 2. MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto la bahari katika eneo la kati la Bahari ya Pasifiki iko chini ya wastani na inatarajiwa kuendelea kuwa chini ya wastani katika kipindi chote cha msimu. Hali hii inaashiria uwepo wa La Niña. Eneo kubwa la Bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la wastani. Hata hivyo, joto la juu kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kusini magharibi mwa Bahari ya Hindi hususan katika miezi ya Novemba, 2020 hadi Januari, 2021. Hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa katika maeneo hayo na upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya kusini mwa nchi.

Katika eneo la mashariki mwa Bahari ya Atlantiki (karibu na Pwani ya Angola), joto la bahari linatarajiwa kuwa la wastani na hivyo kuwa na mchango hafifu kwenye ukanda mvua katika maeneo ya magharibi mwa nchi.

## 3. ATHARI NA USHAURI

Kipengele hiki cha athari na ushauri kimeandaliwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa kwa kushirikiana na wataalam wa sekta husika katika mkutano wa wadau wa hali ya hewa uliofanyika tarehe 19 Oktoba, 2020.

### a) Kilimo na Usalama wa Chakula

Katika kipindi cha mvua za 'Msimu' (Novemba, 2020 hadi Aprili, 2021) hali ya unyevunyevu wa udongo kwa ustawi wa mazao na upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi. Hata hivyo, mazao yanaweza kuathiriwa na hali ya unyevunyevu wa kupitiliza, mmomonyoko wa udongo, kupotea kwa rutuba na kutuama kwa maji mashambani, hususan kwa maeneo yanayotarajiwa kuwa na mvua za wastani hadi juu ya wastani. Aidha, uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji unaweza kujitokeza kutokana na vipindi vifupi vya mvua kubwa vinavyoweza kujitokeza.

Uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua uzingatiwe kwa matumizi katika vipindi vya ukavu vinavyoweza kujitokeza. Pia, mbinu za kuhifadhi unyevunyevu wa udongo zinashauriwa kutumika hasa katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Wakulima wanashauriwa kuwa na miundombinu rafiki ya kusafirisha na kuhifadhi mazao baada ya kuvuna kuepuka uharibifu unaoweza kujitokeza kutokana na hali ya mvua na unyevunyevu unaotarajiwa. Aidha, wakulima wanashauriwa kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalam wa kilimo ikiwa ni pamoja na maafisa ugani katika maeneo yao.

### b) Mifugo na Uvuvi

Hali ya malisho na upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo vinatarajiwa kuwa vya kuridhisha katika maeneo mengi. Aidha, kutakuwa na maji ya kutosha katika maziwa, mito na mabwawa na hali hiyo inatarajiwa kuchangia kuongezeka kwa chakula cha samaki na hivyo kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mazao ya uvuvi. Aidha, magonjwa ya mifugo yanaweza kujitokeza kutokana na vipindi vya mvua nyingi kama vile homa ya bonde la ufa, kuoza kwa kwato na magonjwa yaenezwayo na kupe pamoja na minyoo. Inashauriwa hatua za kuimarisha miundombinu ya ufugaji wa samaki hasa kwenye mabwawa zichukuliwe. Pia, wakulima wa mwani wanatakiwa kuwa na tahadhari dhidi ya magonjwa yanayoweza kujitokeza wakati wa mvua nyingi. Pamoja na utabiri huu wa msimu, wavuvi wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa hali ya hewa unaotolewa mahususi kwa matumizi katika maziwa makuu na bahari. Wafugaji wanashauriwa kutumia mbinu za ufugaji bora na uvunaji maji ya mvua na kuhifadhi malisho kwa ajili ya matumizi ya baadae. Wafugaji na wavuvi wanashauriwa pia kupata ushauri zaidi kutoka kwa wataalam wa mifugo na uvuvi katika maeneo yao.

### c) Utalii na Wanyamapori

Hali ya malisho na maji ya kutosha kwa wanyamapori inatarajiwa kuongezeka hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya barabara, madaraja na maji ili kuimarisha shughuli za utalii.

### d) Usafirishaji

Kutokana na utabiri uliotolewa, miundombinu ya usafirishaji ikiwa ni pamoja na barabara na madaraja, inaweza kuathirika hususan katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Aidha, shughuli za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji zinaweza kuathiriwa. Mamlaka husika zinashauriwa kuboresha miundombinu ya usafirishaji na kuchukua tahadhari stahiki ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na matukio ya mvua kubwa.

### e) Nishati, Maji na Madini

Maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani yanatarajiwa kuwa na ongezeko la kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito. Hali hiyo inaweza kupelekea mito kufurika na kusababisha mafuriko katika maeneo ya mabondeni.

Hata hivyo, matumizi sahihi ya rasilimali maji kwa ajili ya uchakataji wa madini, uzalishaji wa

umeme, matumizi ya viwandani na majumbani yazingatiwe. Aidha, jamii ichukuwe tahadhari ili kuepuka madhara yatokanayo na kuharibika kwa miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme. Jamii inashauriwa kuwepo na matumizi sahihi ya rasilimali maji na kuhifadhi maji kwa ajili ya matumizi ya baadae.

**f) Mamlaka za Miji**

Vipindi vifupi vya mvua kubwa vinaweza kusababisha kutuama kwa maji na mafuriko na kupelekea uharibifu wa miundombinu na upotevu wa maisha na mali. Mamlaka za miji Pamoja na wadau wengine wanashauriwa kuboresha mifumo ya kupitisha maji taka na kuisimamia ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mafuriko. Pia, wakazi wa maeneo hatarishi wanahimizwa kuchukua tahadhari.

**g) Afya**

Hali ya maji kutuama inaweza kujitokeza na kutengeza mazalia ya wadudu wadhurifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji kama vile mabwawa na visima vifupi. Pia, hali hii inaweza kusababisha milipuko ya magonjwa yanayohusiana na maji na wadudu wadhurifu. Hivyo, sekta husika zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuhakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba vya ziada katika vituo vya kutolea huduma za afya endapo itatokea miundombinu kuharibika. Pia, jamii inashauriwa kutibu maji ya kunywa, kuzuia na kuharibu mazalia ya mbu, kuzingatia matumizi sahihi ya vyoo, kuendeleza tabia ya kunawa mikono kwa sabuni na maji tiririka na kudumisha usafi wa mazingira. Aidha, kwa maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani, jamii inaweza kulazimika kutumia maji yasiyo safi, ushauri unatolewa kwa wananchi kutibu maji kabla ya kuyatumia. Msisitizo unatolewa kwa mamlaka husika na jamii kwa ujumla kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari hasi zinazoweza kujitokeza.

**h) Menejimenti za Maafa**

Katika maeneo yanayotarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani, mamlaka husika na kamati za maafa za mkoa, wilaya, kata na vijiji/mitaa zinashauriwa kuchukua hatua stahiki ili kuzuia na kupunguza athari za mvua kubwa zinazoweza kujitokeza.

**i) Vyombo vya Habari**

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta inayohusika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa jamii. Vyombo vya habari vinashauriwa kutafuta na kutumia ushauri wa kisekta kutoka kwa watoa taarifa wa sekta mbalimbali zinazotumia taarifa za hali ya hewa ili kuujulisha umma athari za kisekta. Aidha, vyombo vya habari vinashauriwa kuandaa na kusambaza makala za kitaaluma zenye lengo la kuhabarisha jamii juu ya matumizi sahihi ya utabiri wa hali ya hewa. Pia, vyombo vya habari vinashauriwa kutumia lugha nyepesi na inayoeleweka kwa urahisi kwa watumiaji wa taarifa za hali ya hewa.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

***Angalizo:*** *Mwelekeo wa mvua uliotolewa umezingatia zaidi kipindi cha msimu (miezi sita) na hali ya mvua katika maeneo makubwa. Hivyo, viashiria vinavyochangia mwenendo wa mifumo ya mvua na mabadiliko ya muda mfupi katika maeneo madogo vitazingatiwa katika uchambuzi wa utabiri wa muda wa kati na mfupi. Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na mwezi kama unavyotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.*

**Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa mirejesho ya mwelekeo wa mvua nchini kadri inavyohitajika. Aidha, wadau wanashauriwa kuwasiliana na Mamlaka ili kupata taarifa mahsusi za utabiri wa msimu ili kukidhi mahitaji maalum katika sekta zao.**

JARIDA LA HABARI
ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga
Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# USAFIRI WA ANGA: HUDUMA ZA HALI YA HEWA NI ZA VIWANGO VYA KIMATAIFA

**Kilimanjaro,**

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imekutana na wadau wa huduma za hali ya hewa katika sekta ya usafiri wa anga ili kupata mrejesho wa wadau na maoni yao katika kuendeleza uboreshaji wa huduma hizo kitaifa na kimataifa.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Hamza Kabelwa ambaye pia ni Mkurugenzi wa Utabiri,TMA alieleza kuwa huduma za hali ya hewa kwenye sekta ya usafiri wa anga ni za viwango vya kimataifa kwa vile Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inamiliki cheti cha ubora cha ISO 9001:2015.

“Sambamba na kumiliki cheti cha ubora cha viwango vya kimataifa ambacho iliifanya TMA kuwa nchi ya tatu katika bara la Afrika kumiliki checti hicho mwaka 2017, Mamlaka imeendelea kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na mifumo wa usambazaji wa taarifa za hali ya hewa kwa marubani, waongoza ndege na watoa huduma katika maeneo ya viwanja vya ndege”.

Serikali katika kuboresha miundombinu ya hali ya hewa kwa kusimika mitambo ya kisasa kama vile rada za hali ya hewa, ambapo TMA imetengewa bajeti ya rada mbili zitakazo fungwa Kilimanjaro na Dodoma, zoezi hili litaanza mara baada ya rada za Mbeya na Kigoma kukamilika.

“TMA inatambua sana mchango wa wadau katika kuboresha huduma za hali ya hewa hususani kupitia maoni yanayotufikia kupitia njia mbalimbali, hivyo basi napenda kuwajulisha kwamba TMA imeendelea kupiga hatua chanya kwa kupitia maoni yenu”. Alizungumza Dkt. Kabelwa.

Aidha, wadau walipata fursa ya kupata mrejesho wa namna maoni yao yalivyofanyiwa kazi pamoja na kupata elimu ya masuala mbalimbali ya huduma za hali ya hewa kwenye sekta ya usafiri wa anga, Vile vile waliipongeza TMA kwa uboreshaji wa huduma zake.

Mkutano huo wa wadau ulifanyika katika ukumbi wa mikutano wa KADCO, uliopo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) na kuhudhuriwa na wadau thelathini (30) kutoka katika Taasis za Serikali, Mashirika ya Ndege na wataalam kutoka TMA.




*Wadau wa huduma za hali ya hewa katika sekta ya usafiri wa anga katika picha ya pamoja na mgeni rasmi, mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dkt. Hamza Kabelwa ambaye pia ni Mkurugenzi wa huduma za Utabiri TMA (katikati), wakati wa mkutano uliofanyika KIA.*

JARIDA LA HABARI

TMA TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# WACHIMBAJI MADINI WATAKIWA KUTUMIA TAARIFA MAHSUSI ZA HALI YA HEWA KUONGEZA TIJA NA UFANISI.

**Dodoma,**




*Wachimbaji wakubwa na wa kati kutoka katika sekta ya madini wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi kwenye Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Madini kuhusu Umuhimu wa Huduma za Hali ya Hewa*




*Wachimbaji wadogo kutoka katika sekta ya madini wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi kwenye Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Madini kuhusu Umuhimu wa Huduma za Hali ya Hewa*

Wadau kutoka sekta ya madini nchini wametakiwa kutumia taarifa mahsusi za hali ya hewa ili kuweza kuongeza tija, ufanisi na usalama katika shughuli zinazohusiana na utafutaji, uchimbaji madini na uedeshaji wa migodi.

Matakwa hayo yalitolewa na mgeni rasmi wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Madini kuhusu Umuhimu wa Huduma za Hali ya Hewa, Mhandisi, Aron Kisaka ambaye alifungua mkutano huo akimwakilisha Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi).

"Taarifa sahihi za hali ya hewa zikiwafikia wachimbaji kwa wakati, zitasaidia kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa na kupanga mipango ya kukabiliana na majanga ndani ya sekta yatokanayo na hali mbaya ya hewa kama vile maporomoko ya udongo". Alizungumza Mhandisi Kisaka.

Aidha, Mhandisi Kisaka aliwataka washiriki wa mkutano huo kutoka na uelewa chanya kuhusu sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya mwaka 2019 hususan uhusiano wake na sekta ya madini.

Awali, wakati akimkaribisha mgeni rasmi, Dkt. Agnes Kijazi, Mkurugenzi Mkuu wa TMA na Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) aliwashukuru wadau kwa kuitikia mwaliko na kueleza kuwa Mamlaka inatoa huduma mahsusi kwaajili ya sekta mbali mbali nchini ikiwa pamoja na sekta ya madini, hata hivyo wadau katika sekta ya madini bado hawazitumii ipasavyo huduma hizo. Dkt. Kijazi aliomba washiriki wa mkutano kutumia fursa ya mkutano huo kuelewa huduma mbali mbali zinazotolewa na TMA na kuweka mkakati wa kuzitumia.

"Mkutano huu utakuwa ni fursa muhimu ya kujengeana uelewa kuhusu umuhimu wa huduma za hali ya hewa katika sekta ya madini na faida zitakazopatika endapo huduma hizo zitatumiwa ipasavyo". Alisema Dkt. Kijazi

Naye, Mwakilishi wa Mwenyekiti wa Bodi ya TMA, Bw. Robert Sunday alielezea umuhimu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kukutana na wadau wa sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya madini. Alifafanua kwamba kwa vile Tanzania kupitia Dkt.Kijazi inashika nafasi ya makamu wa tatu wa rais wa WMO ni muhimu nchi yetu ikawa kielelezo katika utumiaji wa taarifa za hali ya hewa katika sekta za maendeleo ikiwemo sekta ya madini. Aidha, alimshukuru mgeni rasmi kwa hotuba nzuri yenye lengo la kujenga na aliwashukuru washiriki wa mkutano huo hususan wadau wa sekta ya madini kwa ushiriki wao.

Kwa upande wa mwakilishi wa wachimbaji madini, Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la Wachimbaji Tanzania (FEMATA) na Kamishna kutoka Tume ya Madini, Bw. Haroun Kinega aliishukuru TMA kwa kushirikiana na Tume ya Madini kuandaa mkutano huo muhimu ambao utaleta mwanga kwa wachimbaji wote kwa ujumla juu ya matumizi sahihi ya taarifa za hali ya hewa. Alikiri kwamba taarifa za hali ya hewa ni za muhimu sana katika sekta ya madini.

Mkutano huu uliofanyika katika ukumbi wa LAPF, Dodoma, Tarehe 08 Disemba 2020, umewakutanisha wadau mbalimbali katika sekta ya madini wakiwemo wachimbaji wakubwa, wakati na wadogo, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Madini, Tume ya Madini, NEMC na TMA.

JARIDA LA HABARI

TMA Tanzania Meteorological Authority

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# ONGEZEKO LA HALI YA JOTO KWA BAADHI YA MAENEO NCHINI

**Dar es Salaam,**



Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) inatoa taarifa juu ya hali ya ongezeko la joto katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Kwa kawaida kipindi cha miezi ya Oktoba hadi Machi kila mwaka jua la utosi linakuwa katika maeneo ya kizio cha kusini mwa dunia. Tanzania ikiwa ni moja ya nchi zilizopo katika kizio cha kusini, huwa na hali ya joto kali katika maeneo mengi ikilinganishwa na miezi mingine. Hapa nchini, vipindi vya jua la utosi vinafikia kilele kati ya mwishoni mwa mwezi Novemba wakati jua la utosi likiwa linaelekea kusini (Tropiki ya Kaprikoni) na hali hiyo hujirudia tena mwezi Februari wakati jua la utosi likiwa linaelekea kaskazini (Tropiki ya Kansa). Jua la utosi huambatana na hali ya Joto kali kwa sababu kipindi hicho ndipo uso wa dunia katika eneo tajwa huwa karibu zaidi na jua kuliko maeneo mengine.

Nyakati za usiku pia kunaonekana kuwa na hali ya joto kutokana na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha unyevunyevu angani kinachofika asilimia themanini na zaidi kwa baadhi ya maeneo. Unyevunyevu huo hutunza hali ya joto litokanalo na mionzi ya jua na hivyo kuleta hali ya fukuto.

Katika kipindi hiki cha mwezi Disemba, 2020 upungufu wa mvua unatarajiwa kujitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata mvua za Vuli (ukanda wa ziwa Viktoria, nyanda za juu kaskazini mashariki pamoja na pwani ya kaskazini). Hali hii inatarajiwa kuendelea kusababisha uwepo wa hali ya joto katika maeneo hayo. Hata hivyo, hali ya joto inatarajiwa kupungua kidogo katika kipindi cha mwezi Januari, 2021 kutokana na mvua zinazotarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha, vipindi hivi vya joto vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika mwezi Februari 2021 wakati jua litakapokuwa la utosi hapa nchini.

Baada ya kipindi hicho hali ya joto inatarajiwa kuanza kupungua hasa kuelekea mwezi Machi ambapo mtawanyiko wa mvua unatarajiwa kuongezeka katika maeneo yanayopata mvua za msimu na kuanza kwa msimu wa mvua za masika.

Taarifa za mwenendo wa joto, zinaendelea kutolewa katika utabiri wa kila siku na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, hivyo tunatoa wito kwa wananchi kuendelea kufuatilia taarifa hizo na kuchukua hatua stahiki kila inapobidi.

JARIDA LA HABARI

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# TMA YATOA MSISITIZO KWA WADAU KUTUMIA VIZURI TAARIFA ZILIZOBORESHWA ZA HALI YA HEWA

**Tanga na Simiyu,**




*Wadau wakiwa kwenye picha ya pamoja katika warsha ya wadau kutoka sekta mbalimbali inayohusu kushirikisha wadau katika uzalishaji wa taarifa za hali ya hewa zilizoboreshwa kwa matumizi katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, zikiwemo za kilimo, uvuvi, maji, nishati na usimamizi wa majanga, iliyofanyika katika ukumbi wa Bandari House, Tanga kuanzia Tarehe 26-27 Novemba, 2020.*

Mamlaka ya Hali ya Hewa imetoa msisitizo kwa wadau kuhusiana na matumizi ya taarifa za hali ya hewa zilizoboreshwa. TMA ilisisitiza hayo wakati wa warsha ya siku mbili kati ya waandaaji na watumiaji wa taarifa za hali ya hewa iliyofanyika mikoa ya Tanga, Manyara, Dodoma na Simiyu, kuanzia tarehe 26 Novemba 2020 mpaka tarehe 8 Disemba 2020. Warsha hiyo ilikuwa na lengo la kushirikisha wadau katika uzalishaji wa taarifa za hali ya hewa zilizoboreshwa kwa matumizi katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, zikiwemo za kilimo, uvuvi, maji, nishati na usimamizi wa majanga.

Warsha hiyo iliandaliwa na TMA ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa WISER (Weather and Climate Information Services for Africa) wenye lengo la kuwaongezea ujuzi wazalishaji na watumiaji wa taarifa za hali ya hewa kwenye sekta mbali mbali ikiwemo kilimo, uvuvi, nishati, maji, na usafiri kwenye maji chini ya udhamini wa Serikali ya Uingereza kwa kushirikiana na taasisi ya hali ya hewa nchini humo.

Aidha, wakati wa warsha hiyo, mambo mbali mbali yalijadiliwa ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa takwimu za hali ya hewa, uandaaji wa taarifa za hali ya hewa za muda mfupi, wa kati na mrefu, usambazaji wa taarifa za hali ya hewa, uandaaji wa taarifa za hali ya hewa kwenye maeneo madogo, lugha, tafsiri na mipaka ya matumizi ya taarifa husika, kupokea mirejesho ya wadau juu ya matumizi ya taarifa za hali ya hewa kwenye maeneo Kwa upande wa washiriki walishukuru Mamlaka kwa juhudi walizozichukua katika kutoa tofauti, pamoja na kuongeza thamani kwa wadau kuweka ushauri na madhara yanayo tarajiwa kwenye taarifa za hali ya hewa zilizo boreshwa.

Pamoja na hayo, washiriki walipata nafasi ya kutoa maoni ya namna bora ya kusambaza taarifa ya hewa ya hewa kwenye maeneo mbalimbali.



*Wadau wakiwa kwenye picha ya pamoja katika warsha ya wadau kutoka sekta mbalimbali inayohusu kushirikisha wadau katika uzalishaji wa taarifa za hali ya hewa zilizoboreshwa kwa matumizi katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, zikiwemo za kilimo, uvuvi, maji, nishati na usimamizi wa majanga, iliyofanyika katika ukumbi wa Double S, Simiyu kuanzia Tarehe 07-08 Disemba, 2020.*

# JARIDA LA HABARI

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)


## KONA YA MTEJA

## MVUA ZA WASTANI NI NINI?

Mvua za wastani ni kiwango cha kawaida cha mvua kinachopatikana katika eneo husika kulingana na wastani wa mvua wa muda mrefu.





**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA:**

Mhariri
Dkt. Agnes Kijazi

Mhariri msaidizi
Monica Mutoni

Waandishi
Monica Mutoni
Rehema Maxmin

Msanifu Kurasa
Kennedy Mgeta


## ELIMIKA NA KIBONZO




- *Jamii/Umma: Umuhimu wa taarifa za hali ya hewa kwa umma ni kulinda na kuokoa mali na maisha pamoja na kuboresha mipango ya kiuchumi na kijamii. Taarifa zinazotolewa kwa umma ni pamoja na utabiri wa hali ya hewa wa muda mrefu na mfupi (msimu, mwezi, siku tano, siku kumi, , kila siku, na ule unaotolewa kulingana na mahitaji ya mteja bila kusahau tahadhari za hali mbaya ya hewa na ushauri kama vile vimbunga, mvua nyingi/mafuriko, n.k.*

© Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania 2018 tanzaniameteorological tmaservices tma_services

JARIDA LA HABARI

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Mwakilishi kutoka kampuni ya Enterprise Electronics Corporation (EEC), Mhandisi. James Youngblood akielezea namna rada inavyofanya kazi wakati wa makabidhiano ya rada ya hali ya hewa Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*




*Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Mhandisi. Aron Kisaka (wa kwanza kushoto), pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi (wa pili kulia) wakiwa katika picha ya pamoja na wawakilishi kutoka kampuni ya Enterprise Electronics Corporation (EEC) Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*



*Mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhandisi. Aron Kisaka (wa kwanza kushoto), pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi (wa pili kulia) wakiwa mbele ya gari iliyokabidhiwa na wawakilishi kutoka kampuni ya Enterprise Electronics Corporation (EEC) Makao Makuu ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*




*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na Makamu wa tatu wa Rais wa Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) Dkt. Agnes Kijazi (wa kwanza kushoto) katika picha ya pamoja na wawakilishi kutoka kampuni ya Enterprise Electronics Corporation (EEC), Bw. Edwin Kisanga(wa katikati) na Mhandisi. James Youngblood, wakionesha mikataba iliyosainiwa baada ya makabidhiano ya rada ya tatu ya hali ya hewa.*

JARIDA LA HABARI

TMA
TANZANIA METEOROLOGICAL AUTHORITY

ISO 9001 2015 CERTECH

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA




*Wawakilishi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi ambaye ni mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhandisi. Aron Kisaka wakati wa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Madini kuhusu Umuhimu wa Huduma za Hali ya Hewa, Dodoma.*




*Wawakilishi kutoka Tume ya Madini wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi ambaye ni mwakilishi wa Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi) Mhandisi. Aron Kisaka wakati wa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Madini kuhusu Umuhimu wa Huduma za Hali ya Hewa, Dodoma.*



*Wadau kutoka wilaya ya Handeni mkoani Tanga wakiwa katika picha ya pamoja na mgeni rasmi ambaye pia ni Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Toba Nguvila kwenye warsha ya kuongeza uelewa wa upatikanaji, kutafsiri matumizi na usambazaji wa taarifa za hali ya hewa katika ukumbi wa FDC, Handeni.*




*Wadau wa sekta ya kilimo na ufugaji walioshiriki katika warsha ya utoaji wa huduma za hali ya hewa iliyofanyika katika wilaya ya Babati wakiwa kwenye picha ya pamoja na mgeni rasmi ndg. Nobert Kyomushula (katikati mwenye shati jeupe).*

JARIDA LA HABARI

ISO 9001: 2015 Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA)

# MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Wawakilishi wa wachimbaji wakubwa na wa kati, wawakilishi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), wawakilishi kutoka Tume ya Madini katika picha ya pamoja na wataalam kutoka TMA, kwenye mkutano mahsusi wa wadau wa sekta ya madini kuhusu huduma za hali ya hewa uliofanyika Makao Makuu ya TMA, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*



*Wawakilishi wa wachimbaji wakubwa na wa kati, wawakilishi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), wawakilishi kutoka Tume ya Madini na wataalam kutoka TMA, katika picha wakipata maelezo kutoka kwa mtaalam wa hali ya hewa kuhusu uhifadhi wa data za hali ya hewa, Makao Makuu ya TMA, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*



*Wawakilishi wa wachimbaji wadogo, wawakilishi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), wawakilishi kutoka Tume ya Madini katika picha ya pamoja na wataalam kutoka TMA, kwenye mkutano mahsusi wa wadau wa Sekta ya Madini kuhusu huduma za hali ya hewa uliofanyika Makao Makuu ya TMA, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*



*Wawakilishi wa wachimbaji wadogo, wawakilishi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), wawakilishi kutoka Tume ya Madini katika picha wakipata maelezo kuhusu studio ya TMA walipotembelea ofisi za Kituo Kikuu cha Utabiri, Ubungo Plaza, Dar es Salaam.*